

8. HANGAIKIA KUWA BORA KATIKA FANI YAKO

Muwe basi na tamaa ya kupata vipaji muhimu zaidi. 1Wakorintho 12:31Kuna mtu alisema, “**Usitafute mafanikio tafuta kuwa mtu mwenye thamani, jithaminishe na watakulipa kwa hilo.**”

Siku moja nilikuwa na semina kule Morocco Kinondoni Dar-Es-Salaam, nikakutana na kijana mmoja akaniuliza, “nifanye nini ili nipate fedha nyingi katika kazi yangu ya umakenika? Mimi nilimwambia ukitaka kupata fedha katika shughuli zako hakikisha unajua kazi kiasi cha kuwazidi mafundi wengine wote wa jiji hili la Dar-Es-Salaam. Alishangaa sana na kucheka. Kwa kweli ukitaka kupata fedha nyingi katika kazi au huduma unayotoa ni lazima uwe juu kwa ubora. Wale walioko juu sana kwa ubora ni wachache sana. Mara nyingi watu hawa hugombaniwa kwa vile kila mtu anapenda kupata huduma kutoka kwa mtaalamu. Richard Kiyosaki aliwahi kusema, “**kijana usifanye kazi kwa ajili ya mshahara bali fanya kazi kwa ajili ya kuijua kazi sana na kuwa mtaalamu.**” Wengi walikuwa wanafanya kazi chini ya watu wengine halafu baadaye waliacha na kuanzisha ofisi zao au kampuni zao. Hii ilitokea baada ya miaka mingi ya kujifunza kazi. Kila unayemwona ambaye ana kampuni yake wengi walianza chini wakiwa hawana kitu ila walikuwa na ujuzi na uaminifu ambaao ulivuta wateja. Ukiwa na ujuzi ni wazi utakuwa na wateja wengi ambaao wanazithamini kazi zako na ujuzi wako na hivyo ukianzisha ofisi yako watakuftuata. Nakumbuka mwalimu mmoja ambaye baada ya kuanzisha shule yake binafsi, wazazi wengi waliwahamisha watoto wao kutoka shule aliyokuwa akifundisha na kuwapeleka katika shule yake mpya.

Yaani wazazi na wanafunzi walimfuata mwalimu huyo kwa sababu ya kuthamini ubora wake. Mjasiliamali mashuhuri, Jeff Hoffman aliwahi kusema, “**usifukuzie fedha, fukuzia kuwa na uwezo wakufanya kazi**

katika ubora wa hali ya juu sana, kwa sababu fedha hufuataubora.”

Fanya jitihada ya kupata ujuzi wa hali ya juu ili wateja wengi wakufuate. Ujuzi wako ndio utakaokutangaza, mteja atakuletea mteja mwingine. Jilizile wewe unategemewa na watu wengine hata na mwajiri wako kwa kiasi gani? Wewe unajipa thamani gani katika kazi yako? Kama ungemuwambia mwajiri wako kwamba wewe unataka kuacha kazi je angekuomba usiache kwa vile anakutegemea au angesema wewe acha tu. Kumbuka huduma au kazi inayofanywa na mtaalamu malipo yake ni ya juu sana. Hivyo, kazi yako yoyote iboreshe. Kama ni huduma iwe juu, kama unafanya huduma yako katika mazingira duni utalazimika kuyaboresha na uwe na ndoto ya kuboresha bidhaa au huduma zako. Jaribu kuhudhuria semina, kusoma majarida na vitabu ambavyo vinaelezea kazi yako au huduma yako. Sikiliza Redio na tazama Televisheni ili ujifunze kitu unachotaka, ikiwezekana hudhuria chuo au kozi fupi kuhusu kazi au huduma yako. Josh Waitzkin alisema, “**Ufunguo wa kutafuta kufanya vizuri sana nikukumbatia mtindo wa kiasili wa kujifunza kwa muda mrefu na siyo kuishi katika ganda la kusimama bila kukua, usalama wa kuogopa hali hatarishi na maisha dhaifu. Mara nyingi kukua kunabebwa na gharama ya kutulia kulikopita na usalama uliopita.**”

Watu wengi wapo tayari kutoa maelfu ya fedha kwa ajili ya starehe badala ya kununua tiketi ya kuingia kwenye semina ya kuongeza ujuzi wao au kununua kitabu kinachoweza kuwaongezea ujuzi.

Kama ni mama yuko tayari kununua puto kubwa kwa ajili ya mwanae kuliko kwenda kununua kitabu au kujifunza zaidi juu ya kazi au huduma anayoitoa ili aongeze kipato zaidi. Katika miaka hii ya utandawazi ndiyo hatari zaidi.

Hivyo yapo mengi ambayo huwa unayahangaikia katika maisha yako ingawa hayakusaidii chochote kimaisha kwa ujumla Yaache sasa fikiri, chagua na fanya yale ambayo yatakufanya uwe bora zaidi katika kazi unayoifanya na ambayo watu wengi hawana ujasiri wa kuyafanya

Ingawa kitendo cha kuyaacha kinahitaji ujasiri mkubwa lakini wewe uwe mtu jasiri namba moja. Usikubali kubaki pale pale miaka yote. Usiseme tu kwa maneno, tenda, chukua hatua jiboreshe na utaona maisha yako yanaboreka zaidi. Napenda kuyarudia maneno ya Jim Rohn aliyoyasema, “**usitamani kiwe rahisi, tamani uwe bora kwa vile mafanikio ni kitu ambacho unakivuta kwa ubora ulionao.**” Fikiria kujiboresha kwanza, usifikirie mapato kwani mapato yatakufluata. Kwa mfano, mtu akiwa na hoteli nzuri pamoja na vyakula vizuri watu husema twende hoteli ile ina chakula kizuri na bila hata kujali gharama yake. Watu hupeleka fedha kwa mwenye hoteli. Jeubora utaupata wapi kama hujaamua kuhudhuria semina, kusoma machapisho na vitabu vinavyohusiana na shughuli zako. Pia ongea na wenye mawazo chanya na waliofanikiwa kwani wao watakupa msukumo mpya. Kuanzia sasa amua kutumia Radio, Televisheni, mitando ya kijamii na interneti kujiangzea ubora badala ya starehe. Usivitumie kwa starehe za muda ambazo zinakudidimiza chini ingawa zinaonekana kama za maana na zinafanywa na wengi. Kitu kikifanywa na wengi haina maana kwamba wanapata faida, wengi hufuata starehe tu. Kuna mtu aliwahi kusema, “**ingawa technologia imekuja kuwasaidia watu lakini pia imekuja kuwaangamiza wengi.**”

Jaribu kuwa miongoni mwa watu wachache ambao wamegundua kwamba tekinologia mpya imepanua uwezo wa kujifunza na kuelimika. Jiulize je mimi teknologia inanilettea faida gani hasa? Kama

wanafunzi wanasomea miaka kadhaa tu fani fulani itakuwaje wewekama utatumia maisha yako kusoma katika fani au shughuli inayoukingizia kipato?

Jamaa mmoja alikuwa anafanya operasheni fulani nchini Marekani akasikia kuwa kule Hongkong kulikuwa na semina inayohusu kazi yake. Aligharamia safari yake toka Marekani hadi huko Hongkong. Na aliporudi nchini mwake alianzisha huduma hiyo mpya ambayo hakuna mwingine aliyekuwa anaitoa na hivyo aliwatoza watu kiasi cha fedha alichotaka na watu walitoka sehemu za mbali takribani kilometra elfu moja kufuata huduma hiyo. Hivyo baada ya kufanya kazi kwa muda wa miaka kadhaa na kuwa milionea aliamua kustaafuli akiwa na miaka hamsini na tatu akiwa na fedha nyingi. Ongeza ujuzi ili uongeze ubora wako wa huduma au kazi yako. Gharama ya kitu kizuri ipo juu na wala usitegemee kuna mtu atakuja kukulipia hiyo gharama. Unachokifikiria sasa na kuamua kukifanyia kazi kwa bidii kitakuletea matunda miaka ijayo usiyoijua, mtu mmoja alisema “**mtu anaweza kuhesabu nakujua mbegu zilizo katika tunda la tofaa lakini ni MUNGU tu ndiye anayeweza kujua mbegu moja ya tunda la tofaa inaweza kutoa matunda mangapi.**” Hii ndiyo siri ya mafanikio. Uwe na maono angalia juu kuliko na mafanikio. Acha kuangalia chini kuliko na umasikini na kushindwa. Fikiria maisha yako ya baadaye, piga hatua ya ziada. Fanya kazi kubwa kuliko malipo wakati unajifunza, uwe tayari hata kufanya kazi bila malipo, kuwa mvumilivu, mstahimilivu na mwenye imani.

Katika hili Mwinjili Matayo anatuambia, “**mtu akikulazimisha kubeba mzigo wake kwa kilometra moja beba kilometra mbili.**” Matayo 5:41. Fanya zaidi, umia zaidi, Unapoanza kwa kuwa hujulikani, utalazimika kufanya bure, bila malipo kwa muda mrefu ili ujifunze.

Nakutolea ushuhuda wangu mimi mwenyewe nilitoa semina katika shule zaidi ya sabini kwa miaka zaidi ya minne bila malipo yoyote katika jiji la Dar-Es- Salaam na niliongea kwenye Televisheni kwa zaidiya miaka minne bila malipo yoyote. Nayakumbuka maneno ya Papa Yohane XXIII aliyesema, “**usipate ushauri kwenye woga, bali matumaini na ndoto. Usijhusishe na yale ambayo uliyajaribu na kuyashindwa bali jihusishe na ambayo bado yanawezekana kufanywa na wewe.**

Kwa **mfanyakazi** ichukulie kazi unayoifanya kama ni kazi yako binafsi, yaani ichukulie kama umejiajiri. Jua kila kitu kuhusu kazi yako, jitume na uwe na mawazo chanya kuhusu kazi yako. Jiboreshe kwa kupata uzoefu unaokwenda na wakati, usijivunie kupata kazi au kuwa na uzoefu wa miaka mingi, jivunie matokeo mazuri unayoyatoa katika kazi yako. Kwa mfano, lazima mwalimu ujivunie ufaulu wa wanafunzi wako wa darasa unalofundisha na lazima uwe anawahamasisha wanafunzi wako kwa namna mbalimbali. Kama wanafunzi wengi hawaelewi jiulize, “kwa nini wanafunzi wangu hawaelewi? Uangalie mtindo wako uliokuwa unautumia kuwafundishia. Lazima uwe na mahusiano mazuri na wanafunzi wako. Nakumbuka maneno ya George Washington Cover aliyesema, “**kujifunza kokote nikuelewa mahusiano.**” Ni wale ambaa wanajiwajibisha sana na kuichukua kazi kama yao binafsi ndio wanaofaidi matunda ya kazi hiyo. Hao hupewa nafasi ya kwenda kusoma na baadaye huchukua vyeo vya juu katika idara na makampuni. Mitazamo yao inawapeleka juu, hawa hujivunia mishahara yao kuwa ni matokeo ya kazi zao zenye mafanikio.

Fanya kazi kwa bidii na kwa dhamira ya kujifunza zaidi ili kuijua zaidi na ikiwezekana uwe ni mtaalamu wa kazi yako. Kumbuka kiwango kingine cha juu cha kipato unachotaka kinakuhitaji wewe kuwa mtu

wa kiwango cha juu cha ujuzi na utendaji. Leonardo Dicaprio aliwahi kusema, "**Kila kiwango chako cha maisha kinachofuata kinakuhitaji wewe ukiwa tofauti.**" Kua kila siku usikubali kuridhika na kubaki kiwango kile kile cha ujuzi na maarifa. .

Hakikisha wewe unakuwa ni mhimili wa kampuni au taasisi unayofanya kazi. Hapo ndipo utakapoanza kupata matunda makubwa kutokana na kazi yako. Ni baada ya kuwa mfanyakazi stadi, ndipoutaweza kupata mapato makubwa kutokana na kazi yako na pia kuanzisha shughli zako binafsi kwani huwezi kujuua, inawezekana MUNGU anakutayarisha kuja kumiliki kampuni au taasisi yako.

